 Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Atashasta Nditiye (katikati) akizungumza na Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wakati alipotembelea makao makuu ya Mamlaka hiyo jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dkt. Buruhani Nyenzi na kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo Dkt. Hamza Kabelwa	 *Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Atashasta Nditiye (wa pili kushoto) akipatiwa taarifa za namna utabiri wa hali ya hewa unavyofanyika. Kusoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri TMA, Dkt Buruhani Nyenzi na kulia kwake ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu Dkt H. Kabelwa. Wa pili kushoto Naibu Waziri ni Meneja wa Utabiri TMA, Bwana Samwel Mbuya.*

Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Atashasta Nditiye aitaka tma ijitangaze umuhimu wake kiuchumi na kijamii

NDITIYE AITAKA TMA IJITANGAZE UMUHIMU WAKE KIUCHUMI NA KIJAMII

Mnamo tarehe 27 Februari 2018 Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Atashasta Nditiye alitembelea Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Mhandisi Nditiye aliielekeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kujitangaza umuhimu wake katika nyanja ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi na taifa kwa ujumla. Mhe. Nditiye aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na bodi ya Mamlaka hiyo, menejimenti na wafanyakazi kwa lengo la kutambua majukumu yao na kufuatilia utekelezaji wake ili kufikia malengo ya Serikali ya kuwatumikia wananchi.

Akizungumza na Bodi, menejimenti na wafanyakazi, Mhandisi Nditiye aliwaeleza kuwa TMA ni chombo muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya taifa letu na wananchi kwa ujumla kwa kuwa sekta ya usafiri wa anga, majini, ujenzi wa

majengo mbalimbali, miundombinu ya barabara na reli, afya, kilimo na mazingira vyote vinategemea taarifa za hali ya hewa kutoka kwenye Mamlaka hii. “Mtambue kuwa hakuna ndege inayoweza kutua wala kuruka bila kupata taarifa kutoka kwenu, vile vile mkandarasi anayejenga reli ya kisasa ya SGR naye anategemea taarifa zenu kwa kiasi kikubwa, hivyo mtambue ninyi ni muhimu na mjitangaze,” alisema Mhandisi Nditiye.

Alisisitiza kwa kusema kuwa ‘ni vema mjitangaze ili wananchi na wadau mbalimbali wafahamu majukumu na umuhimu wa taasisi yenu kwa kuwa uchumi wa taifa hili unategemea taarifa zenu ambapo wananchi wengi wamezoea kusikia na kuwaona mkitoa taarifa za tahadhari za hali ya hewa zinazohusiana na majanga na matukio mengine yanayohusiana na utabiri wenu angali ninyi mna taarifa muhimu zaidi na tofauti na mtazamo wa wananchi walio wengi’.

Amefafanua kuwa ‘wananchi wanaziamini taarifa zenu za hali ya hewa kwa kuwa kwa kiasi kikubwa yale mnayotabiri na kuwaeleza ndiyo yanayotokea iwe ni mvua kubwa, upepo mkali au joto kali kama ilivyo sasa. Nimetembea na kukagua mitambo, vifaa vya kisasa na namna wanavyofanya kazi na nimebaini kuwa taarifa zinazotolewa hapa zimekusanywa kutoka vituo mbali mbali vya hali ya hewa nchini ambapo hapa makao makuu wataalamu wanazichakata, kusambaza kwa wahusika na kuhifadhiwa, na zinaonesha kuwa ni taarifa za uhakika kwa kiwango cha asilimia 87.5 ambapo imeongezeka kutoka asilimia 82.1 kwa miaka mitatu iliyopita,” amesema Mhandisi Nditiye.

Mwenyekiti wa Bodi ya TMA Dkt. Buruhani Nyenzi wakati akiwasilisha taarifa yake kwa Mhandisi Nditiye amesema kuwa Mamlaka hii ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya taifa letu na wananchi kwa ujumla kwa kuwa utoaji wa taarifa na huduma za hali ya hewa nchini zimewezesha uokoaji wa maisha ya watu na mali zao; kuepuka au kupunguza athari na hasara zinazosababishwa na matukio ya hali ya hewa; kuongeza tija na mafanikio katika shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi; kuwa na miundombinu imara kama vile barabara, madaraja; kuongeza ufanisi katika sekta

za usafiri na mawasiliano; kuchangia katika sekta za ujenzi na uendeshaji wa viwanda nchini na kukuza pato la taifa.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt. Hamza Kabelwa alimueleza Mhandisi Nditiye kuwa wahitaji wa taarifa za hali ya hewa kutoka kwa taasisi na wadau mbalimbali ambao wanahitaji kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii wamekuwa wengi na teknolojia ya utabiri wa hali ya hewa na utoaji wa taarifa zake vimebadilika ambapo inatulazimu kuhuisha Sheria Na. 6 ya Hali ya Hewa ya Mwaka 1978 na kukamilisha Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa ili ziweze kwenda na wakati pamoja na kuboresha chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kwa kuwa ndio chuo pekee nchini kinachotoa elimu ya awali na ya kati ya hali ya hewa.

Aliongeza kuwa TMA imepatiwa cheti cha ubora wa utoaji huduma na Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO) kwa kutoa huduma kwa sekta ya anga nchini. Pia, inashirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa jangwa la Afrika (SADC), Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kwa kubadilishana taarifa za hali ya hewa, mabadiliko ya hali ya hewa yanayohitaji ushirikiano wa kimataifa, na kuendeleza na kutunza mtandao wa vituo vya uangazi wa hali ya hewa ili kukidhi makubaliano ya kimataifa ya kubadilishana taarifa hizo.

Dkt. Nyenzi alimshukuru Mhandisi Nditiye na kumueleza kuwa TMA inafarijika kusikia kuwa anafahamu kwa undani umuhimu wa utabiri wa hali ya hewa nchini, hivyo ni imani yake kuwa ataisamimia vema ili ifikie malengo.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano